# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAJI

## MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI
## WA MAZINGIRA MUSOMA

# MKATABA NA. AE/040/2021/2022/HQ/W/01-AJIRA YA KAZI YA UCHIMBAJI WA MTARO, USAMBAZAJI NA ULAZAJI WA BOMBA PAMOJA NA UFUKIAJI WA MTARO UMBALI WA MITA 6181.20

**KATI YA**

**BW** PAULO CHINI SHIMBA

**NA**

## MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MUSOMA

## (MUWASA)

**MKATABA NA: AE/040/2021/2022/HQ/W/01**

**MRADI WA UPANUZI WA MTANDAO WA MAJI KWA MITAA SABA ISIYOPATA HUDUMA YA MAJI KATIKA MANISPAA YA MUSOMA**

Mkataba huu umefanyika leo tarehe ......15...... Mwezi...11...... Mwaka 20..21......

**Kati ya**

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) S. L. P 233 Musoma ambaye ni "Mwajiri" kwa upande mmoja

**Na**

Bw...Paulo chinishimba...mwenye simu namba ..0763504950..ambaye ni "Mwajiriwa/Mchimbaji wa Mtaro, Msambazaji na Mlazaji wa Bomba na Mfukiaji wa Mtaro" kwa upande mwingine.

1. **AINA YA MKATABA**

   Ajira hii ni ya mkataba wa kazi maalum kwa ajili ya kuchimba mtaro, kusambaza na kulaza bomba pamoja na kufukia mtaro umbali wa mita 6181.2 kwenye mradi wa **UPANUZI WA MTANDAO WA MAJI KWA MITAA SABA ISIYOPATA HUDUMA YA MAJI KATIKA MANISPAA YA MUSOMA**

2. **KUANZA KWA MKATABA**

   Mkataba huu utaanza mara baada ya Mwajiriwa kupokea taarifa rasmi kutoka kwa Mwajiri kuhusu tarehe ya kuanza kwa kazi.

3. **MAHALI/ENEO LA KAZI;**

   Kazi hii ya kuchimba mtaro, kusambaza na kulaza bomba, pamoja na kufukia mtaro umbali wa mita 6181.20 itafanyika kwenye mitaa ya Kwangwa A, Kwangwa B, Bweri Bukoba (Nyamitwebiri), Nyabisarye na Songambele katika Manispaa ya Musoma.

4. **MALIGHAFI ZA UTEKELEZAJI WA KAZI MAALUM**

   Mwajiri atatoa mabomba, viungio na valvu vitakavyotumika katika utekelezaji wa mradi huo pamoja na mashine ya kuunganisha bomba. Vifaa vingine vya kutekeleza kazi atatoa Mwajiriwa.

5. **MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA KAZI**

   Utekelezaji wa mkataba huu utahusisha kazi zifuatazo.

   a) Kuchimba mtaro, kusambaza na kulaza bomba, pamoja na kufukia mtaro wa umbali wa mita 6181.20

6. **GHARAMA YA KAZI MAALUM**

   Gharama ya utekelezaji wa kazi hii itakuwa Fedha za Kitanzania kiasi cha shilingi 39,268,400.00 (Milioni Thelathini na Tisa Mia Mbili Sitini na Nane Elfu Mia Nne tu), kama ilivyochanganuliwa katika jedwali hapo chini;

Jedwali: Mchanganuo wa Gharama za Kuchimba Mtaro, Kusambaza na Kulaza Bomba pamoja na Kufukia Mtaro

| Na. | Aina ya Udongo | Sifa za Mtaro | | Gharama ya kuchimba Mtaro, Kusambaza na Kulaza Bomba pamoja na Kufukia Mtaro kwa kila Mita Moja ya Urefu wa Mtaro (TZS) | Jumla ya Urefu wa mtaro (m) | Gharama kwa Mtaro Wote (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Upana (m) | Kina (m) | | | |
| 1 | Udongo laini usiokuwa na mwamba wa kerege na lukili | 0.45 | 0.9 | 3,000/= | 1000 | 3,000,000/= |
| 2 | Udongo mgumu wenye mwamba wa kerege na lukili | 0.45 | 0.9 | 7,000/= | 5181.2 | 36,268,400/= |
| **Jumla Kuu** | | | | | | **39,268,400/=** |

## 7. UTARATIBU WA MALIPO YA KAZI MAALUM

a) Mwajiriwa atalipwa jumla ya kiasi cha Tshs 39,268,400.00 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kwa awamu kulingana na hatua ya kazi iliyofikiwa;

b) Malipo ya Mwajiriwa yatakuwa ni kwa Fedha za Kitanzania tu.

c) Malipo hayo yatalipwa ama kwa fedha taslim au hundi ambayo italipwa benki;

d) Malipo ya Mwajiriwa yatalipwa kwa awamu kulingana na pendekezo la Msimamizi wa Mradi (Project Manager)

e) Kabla ya malipo ya mwisho kufanyika, Mwajiriwa anapaswa kuwasilisha taarifa zote zinazohitajika na kukabidhi kazi iliyokamilika.

## 8. WAJIBU WA MWAJIRI

Mwajiri ambaye atawakilishwa na Msimamizi wa Mradi, atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kutoa bomba, viungio na valvu vitakavyotumika katika utekelezaji wa mradi.

b) Kusimamia na kuthibitisha ubora wa kazi inayofanywa.

c) Kuwasiliana na uongozi wa eneo husika namna ya kuwashirikisha wananchi katika shughuli za utekelezaji wa mradi

b) Endapo kazi itakayofanywa na Mwajiriwa haitafikia viwango vya ubora unaotakiwa, Mwajiri atachukuwa hatua stahiki dhidi ya Mwajiriwa huyo; na Msimamizi wa Mradi atamtaarifu Mwajiriwa wa kazi hii kwamba ameshindwa kutimiza masharti ya makubaliano.

e) Kuhakikisha kuwa endapo Mwajiriwa atafanya kazi isiyokidhi viwango au isiyoridhisha, Mwajiriwa huyo anarekebisha au kurudia upya kazi hiyo kwa gharama zake mwenyewe.

## 9. MAJUKUMU NA WAJIBU WA MWAJIRIWA

Mwajiriwa ambaye ni...Paulo Chiri Shimba.........atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kuhakikisha kuwa anatekeleza kazi za uchimbaji wa mtaro, usambazaji wa na ulazaji wa bomba, pamoja na ufukiaji wa mtaro kama zilivyoelekezwa kwenye Sehemu ya 1 (Aina ya Mkataba) kulingana na vipimo vilivyotolewa na Mwajiri;

b) Kuhakikisha kuwa anawajibika kufanya kila jambo ambalo kwa ujumla wake litaleta mafanikio kwenye mradi.

c) Atatekeleza majukumu yake kwa uaminifu, uadilifu, umakini na weledi mkubwa na endapo atatekeleza kinyume na matakwa haya, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake;

d) Atawajibika kwa Msimamizi wa Mradi (Project Manager) kwa utendaji wake wa kila siku atatekeleza wajibu kwa kuzingatia maelekezo anayopewa na kiongozi huyo;

e) Atawajibika kuhudhuria mikutano ya tathimini ya kazi yake pamoja na watendaji wengine wa timu yake kila itakapohitajika;

f) Atawajibika kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa kazi yake kila zitakapohitajika;

g) Kuhakikisha malipo ya vibarua walioajiriwa kwa mikataba midogo yanafanyika kwa wakati; na

h) Kufanya usafi ili kuondoa uchafu wote utakaosababishwa na shughuli zake kama itakavyoelekezwa na Msimamizi wa Mradi.

## 10. DHAMANA YA UHARIBIFU

a) Mwajiriwa atawajibika kulipa gharama za uharibifu au madhara yoyote yatakayosababishwa na wafanyakazi wake au vifaa vyake wakati wa utekelezaji wa mradi; na

b) Gharama hizo au madhara hayo yataainishwa na Msimamizi wa Mradi kwa maandishi.

**11. SHERIA ITAKAYOTUMIKA.**

Mkataba huu utaongozwa na kusimamiwa na sheria ya mikataba na sheria nyingine za Tanzania.

**12. UTATUZI WA MIGOGORO**

Endapo kutatokea mgogoro wa aina yoyote baina ya Mwajiri na Mwajiriwa kuhusu utekelezaji wa mradi huu:

a) Pande zote mbili zitatatua mgogoro huo kwa njia ya amani kupitia mazungumzo ambapo makubaliano ya pande hizi mbili yatapelekea Mkataba huu kufanyiwa marekebisho; na

b) Endapo mgogoro huo utashindikana kutatuliwa kwa njia ya mazungumzo, pande zote mbili zinaweza kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa mujibu wa sheria za Tanzania.

**13. KUKOMA KWA MKATABA**

Mkataba huu utafikia ukomo baada ya kazi kukamilika na kukabidhiwa kwa Mwajiri au kwa kusitisha mkataba huu endapo upande mmoja utahusika na ukiukwaji mkubwa wa masharti ya mkataba huu kwa kutoa notisi ya siku 3 bila kuathiri haki ya kila upande.

**14. Masharti mengine katika utekelezaji wa mkataba huu ni kama ifuatavyo:-**

Mwajiriwa atahakikisha kazi zilizoainishwa katika mradi zinatekezwa kila siku bila kusimama.

**15. MAREKEBISHO YA MKATABA**

Kwamba Mwajiri na Mwajiriwa wanaweza kubadilisha baadhi ya masharti ya Mkataba huu kwa makubaliano ya pamoja kwa njia ya maandishi.

**16. KUSAINIWA KWA MKATABA.**

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 15 Mwezi 11 Mwaka 2021

**Kwa Niaba ya Mwajiri:**

Jina: Nicas Mugisha

Sahihi: [signature]

Cheo: Kaimu Mkurugenzi Mtendaji

**Shahidi**

Jina: Burton Kagimu

Sahihi: [signature]

Cheo: Ag. PM

**Mwajiriwa :**

Jina: Paulo Chini Shimba

Sahihi: [signature]

Cheo: Mchimbaji

**Shahidi**

Jina: Amani Makalaji

Sahihi: [signature]

Cheo: Msaidizi